

MAELEZO YA KATIBU MKUU KIONGOZI WAKATI WA BONANZA LA SHIMIWI TAREHE 10 AGOSTI, 2024 UWANJA WA JAMHURI, DODOMA

- **Bw. Juma Mkomi, Katibu Mkuu – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,**
 - **Bw. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Makatibu Wakuu mliopo,**
 - **Viongozi wa SHIMIWI,**
 - **Wakuu wa Taasisi mliopo,**
 - **Watumishi wa Umma na Wanamichezo mliopo,**
 - **Ndugu Wanahabari,**
 - **Mabibi na Mabwana**
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania..... Kazi Iendelee!**

Ndugu Watumishi na Wanamichezo, Kwanza kabisa ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa leo kwa ajili ya bonanza hili lenye lengo la kujiandaa na Michezo ya SHIMIWI iliyopangwa kufanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 18 Septemba hadi tarehe 5 Oktoba, 2024.

Pili, pongezi kwenu watumishi wa umma kwa kutekeleza majumuku yenu na ushiriki wenu kwa ujumla katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

Shukrani kwenu watumishi na wanamichezo ambao mmepata fursa ya kujumuika hapa leo kwa ajili ya kufanya mazoezi ya pamoja, naamini mmewawakilisha wanamichezo wengine wengi. Aidha, ninaishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Shirikisho la Michezo ya Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) kwa maandalizi mazuri ya Bonanza hili,
Hongereni sana!

Shukurani pia kwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Baraza la Michezo la Taifa kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kusimamia na kuratibu michezo nchini. Michezo ni afya na ni fursa hivyo ni vyema Watanzania tuitumie kikamilifu. Nisisitize Wizara yenye dhamana na michezo kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali nchini kuhakikisha Taifa linafanya vizuri katika nyanja ya michezo yote nchini na kimataifa. Pia kipekee ninawashukuru OSHA, NMB na wadau wengine wote mnaodhamini na kuiwezesha SHIMIWI kufanikisha majukumu yake.

Ndugu Watumishi, ninaomba kutumia fursa hii niwakumbushe kwamba sisi ni chachu ya maendeleo ya Taifa letu. Tuna jukumu la msingi katika kuratibu, kuandaa na kutekeleza mipango ya maendeleo ya nchi, hivyo wakati wote tunapaswa kuzingatia mambo yafuatayo; -

- (i) Wakati wote tunapaswa kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora kwa Watanzania;
- (ii) Tunafanya kazi kwa bidii na kwa weledi ili kuleta matokeo chanya;
- (iii) Tunaongeza ubunifu na tija katika shughuli za Serikali ili kuinua ubora wa huduma tunazotoa kwa wananchi; na

- (iv) Tuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma wakati wote tunapotekeleza majukumu yetu;

Ndugu Watumishi, kama sehemu ya jamii, watumishi wa umma lazima tuwe wabunifu katika kushughulikia changamoto na mahitaji ya msingi ya wananchi ili kuandaa mipango bora inayolenga kuinua maisha yao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Ili kutekeleza majukumu haya mazito, Watumishi wa Umma hatuna budi kuwa na afya njema na akili timamu. Masuala haya yanapatikana katika utaratibu bora wa maisha unaozingatia ulaji unaofaa, kufanya mazoezi ya mwili na kuepuka mwenendo wowote hatarishi. Utaratibu huu unasaidia kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu, magonjwa ya moyo, kisukari na magonjwa mengine kama wataalam wa afya wanavyoshauri.

Ndugu Watumishi, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeweka utaratibu maalum wa kusimamia michezo katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ili kutoa fursa kwa watumishi wa umma kushiriki michezo kwa afya. Aidha, michezo inajenga na kuimarisha umoja katika Utumishi wa Umma kwa kuwa watumishi wanapata fursa ya kujumuika pamoja. Bila kuwa na umoja ni vigumu kutimiza malengo ya Serikali, hivyo tutumie fursa ya michezo katika kujenga umoja.

Ndugu Watumishi, ninapohitimisha ninaomba kuendelea kusositiza kuhusu umuhimu wa michezo. Aidha, ninatoa rai kwa waajiri kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za michezo ikiwa ni pamoja na kuwapa watumishi ruhusa za

kuhudhuria michezo na mashindano mbalimbali kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni za Utumishi wa Umma. Vilevile, ni muhimu kuzingatia masuala ya nidhamu tunapokuwa michezoni. Viongozi mahali pa kazi mhakikishe mnasimamia kwa ukamilifu watumishi waweze kufanya mazoezi na kushiriki kwenye michezo kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

Ndugu Watumishi na Wanamichezo, kama mnavyofahamu Mwaka 2024 ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, hivyo nitoe wito kwa watumishi wa umma kushiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi bora.

Ndugu Watumishi, nimalizie kwa kuwapongeza na wote tulioshiriki kwenye Bonanza la leo. Ninawataenia kila la kheri katika Michezo ya SHIMIWI ya mwaka 2024 inayotarajiwa kufanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe **18 Septemba – 5 Oktoba, 2024**.

Asanteni sana kwa kunisikiliza